

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU
MAPENDEKEZO YA NYONGEZA YA BAJETI YA MWAKA 2021/22**

Ofisi ya Bunge
S.L.P 941
DODOMA.

YALIYOMO

1.0.	UTANGULIZI.....	1
2.0.	Chimbuko la Mkopo usio na riba kutoka IMF	2
2.1.	Mpango Mahususi wa Kukabiliana na Athari za Kijamii na Kiuchumi za Uviko-19 (Tanzania Covid-19 Socio-Economic Response and Recovery Plan – RCRP).....	2
2.2.	Dirisha la Mikopo ya Dharura la IMF	3
3.0.	MISINGI YA KISHERIA NA KIKATIBA KUHUSU UWASILISHAJI MAPENDEKEZO YA NYONGEZA YA BAJETI YA MWAKA 2021/22 <i>SUPPLEMENTARY BUDGET</i>	4
3.1.	Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.....	4
3.2.	Sheria ya Bajeti Sura ya 439.....	5
3.3.	Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/22.....	5
4.0.	MGAWANYO WA FEDHA ZA MKOPO	6
4.1.	Majadiliano baina ya Kamati ya Bajeti na Serikali.....	6
4.2.	Mgawanyo wa Mkopo baada ya Majadiliano	8
5.0.	UCHAMBUZI WA MAPENDEKEZO YA NYONGEZA YA BAJETI YA MWAKA 2021/22.	8
5.1.	Uchambuzi wa Makusanyo	8
5.2.	Uchambuzi wa Matumizi.....	9
5.3.	Ujenzi wa Kipande cha Reli cha Makutopora Tabora	11
6.0.	MAONI NA MAPENDEKEZO YA UJUMLA	11
6.1.	Mradi wa Ujenzi wa Vibanda vya Wafanyabiashara wadogo	11
6.2.	Changamoto ya Utilewaji wa Misamaha ya Kodi.....	11
6.3.	Uwazi na Uwajibikaji kwa Mikopo inayochukuliwa na Serikali	12
7.0.	PONGEZI.....	12
8.0.	HITIMISHO.....	13

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU MAPENDEKEZO YA NYONGEZA YA BAJETI YA MWAKA 2021/22

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Awali ya yote kwa niaba ya Kamati naomba kutoa pongozi za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Juhudi zake binafsi katika kuliletea Taifa maendeleo. Kwa Muhtasari naomba nielezee namna ambayo Mheshimiwa Rais ameutanabahisha umma juu ya uongozi wake na mwelekeo wa Taifa.

- i. Kwanza Mheshimiwa Rais ameonyesha nia yake thabiti ya kuwajali Watoto wa kitanzania na hasa wanafunzi kwa kuhakikisha kila aliefaulu na anastahili kwenda shule anapata fursa hiyo bila kikwazo chochote;
- ii. Amedhihirisha umma kwamba ili uboreshe maisha ya watu kwanza lazima uboreshe huduma za msingi za jamii kama afya, elimu, barabara na maji;
- iii. Ameonyesha kwamba inawezekana kushirikisha Bunge katika mgawanyo wa matumizi ya fedha za mikopo inayochukuliwa na Serikali;
- iv. Ameitangazia Dunia namna tofauti ya Tanzania kupambana na Uviko-19 kwa kuangalia huduma muhimu ambazo ama zikikosekana zinaweza kusababisha kusambaa kwa ugonjwa huo zaidi au endapo mtu ataupata atakosa huduma muhimu ili kuokoa maisha yake;
- v. Amethibitisha kwa Watanzania kauli mbiu yake ya “Kazi lendelee” na Watanzania wameona kazi inaendelea; na
- vi. Ameuthibitishia ulimwengu kwamba Tanzania sio kisiwa ni lazima ishirikiane na mataifa mengine ili kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Bila kupepesa macho wala ajizi naomba kurejea kauli ya Watanzania kwamba Mama Anaupiga Mwingi. Kamati inaamini hakuna Mbunge yeyote alieko katika ukumbi huu atakaepinga matumizi ya mkopo huo kwa sababu manufaa yake yanaonekana nchi nzima.

2.0. Chimbuko la Mkopo usio na riba kutoka IMF

2.1. Mpango Mahususi wa Kukabiliana na Athari za Kijamii na Kiuchumi za Uviko-19 (Tanzania Covid-19 Socio-Economic Response and Recovery Plan – RCRP).

Mheshimiwa Spika, Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (World Health Organization – WHO) liliutangaza Ugonjwa wa Homa ya Mapafu unao sababishwa na Virusi vya COVID-19 Tarehe 11 Machi, 2020¹ kama janga la Dunia. Janga hili limesababisha matatizo mbalimbali ya kiuchumi na kijamii Duniani na kwa Tanzania. Kutokana na Madhara hayo Tanzania iliandaa Mpango ujulikanao kama Mpango Mahususi wa Kukabiliana na Athari za Kijamii na Kiuchumi za Uviko-19 (*Tanzania Covid-19 Socio-Economic Response and Recovery Plan – RCRP*)². Utekelezaji wa Mpango huo ulitarajiwa kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 3.62**. Lengo kubwa la Mpango huo ni kuzisaidia sekta mbalimbali za kiuchumi zilizo athirika na Uviko -19 pamoja na kupunguza maambukizi kwa binadamu. Hivyo, katika utekelezaji wa Mpango huo ndipo Serikali iliomba Fedha Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na kupewa kiasi cha jumla ya **Dola za marekani milioni 567.3**.

¹ Virtual press conference on COVID-19 – 11 March 2020

²reliefweb.int/sites/reliefweb.int/files/resources/EHoA%20%20COVID19%20Strategic%20Response%20and%20Recovery%20Plan%202021_0.pdf

2.2. Dirisha la Mikopo ya Dharura la IMF

Mheshimiwa Spika, Dirisha la Mikopo ya Dharura (*Rapid Credit Facility - RCF*³) ni dirisha ambalo hutoa usaidizi wa haraka wa kifedha wenye masharti nafuu kwa nchi za kipato cha chini (*Lower Income Countries-LICs*) zinazokabiliwa na nakisi kubwa kwenye urari wa malipo ya jumla (*Balance of Payment Deficit*). Dirisha hili liliundwa chini ya Mfuko wa Kupunguza Umaskini na Kukuza Uchumi (*Poverty Reduction and Growth Trust-PRGT*)⁴. Lengo kubwa la dirisha hili ni kutoa usaidizi wa kifedha kwa nchi za kipato cha chini kwa urahisi zaidi ili ziweze kupambana na matatizo ambayo yanakabili chumi ili kupunguza umasikini.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa Namba 21/213⁵ ya Shirika la Fedha la Kimataifa iliyotolewa na Bodi ya Shirika hilo tarehe 7 Mwezi Septemba Mwaka 2021 ambayo ilitokana na Taarifa ya hali ya Uchumi wa Tanzania ilioandaliwa na Maafisa wakazi wa Benki hiyo waliopo nchini. Taarifa hiyo ilibainisha maeneo ya uchumi yaliyoathirika na ugonjwa wa homa kali ya mapafu na hivyo Taifa lilihitaji msaada wa kifedha ili kupambana na athari hizo. Baadhi ya Sababu hizo ni kama ifuatavyo: -

- i. Kushuka kwa ukuaji wa uchumi wa Taifa kutoka **asilimia 6.9** mwaka 2019 hadi **asilimia 4.8** mwaka 2021;
- ii. Kuathirika kwa Sekta ya Utalii ambapo idadi ya watalii wanaoingia nchini ilishuka kwa **asilimia 60** kati ya mwaka 2019 na 2021;
- iii. Watu zaidi ya **140,000** kutoka katika ajira rasmi na wasiopungua **1,000,000** wa sekta isiyo rasmi walipoteza ajira zao na hivyo kupelekeea ongezeko la watu masikini kwa **asilimia 0.6** kutoka **asimilia 26.5** hadi **asilimia 27.1**;
- iv. Kushuka kwa mapato ya Serikali kwa **asilimia 2.5** ya Pato la Taifa;

³ <https://www.imf.org/en/About/Factsheets/Sheets/2016/08/02/21/08/Rapid-Credit-Facility>

⁴ <https://www.imf.org/en/About/Factsheets/IMF-Support-for-Low-Income-Countries>

⁵ <https://www.imf.org/en/Publications/CR/Issues/2021/12/02/United-Republic-of-Tanzania-Request-for-Disbursement-under-the-Rapid-Credit-Facility-Press-510749>

- v. Urari wa malipo ya kawaida uliathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na kushuka kwa mapato ya utalii kwa **asilimia 55** na kushuka kwa mauzo nje ya Mazao ya Biashara ya Pamba, Kahawa na Tumbaku kwa **asilimia 40**;
- vi. Akiba ya Fedha za Kigeni ilipungua kutoka **Dola za Marekani Billioni 5.6** mwaka 2019 hadi **Billioni 5.2** mwaka 2021; na
- vii. Kushuka kwa Mikopo kwa Sekta Binafsi kutoka **asilimia 11** Mwaka 2019 hadi **asilimia 2.3** mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, kwa pamoja sababu hizo zilipelekea kuwa na nakisi kubwa kwenye Urari wa Malipo ya Jumla. Hivyo mkopo huo ultolewa ili uje kuchochea ukuaji wa uchumi pamoja na kupunguza nakisi ya Urari wa Ujumla. Mgawanyo wa fedha hizi umethibitisha lengo hilo.

3.0. MISINGI YA KISHERIA NA KIKATIBA KUHUSU UWASILISHAJI MAPENDEKEZO YA NYONGEZA YA BAJETI YA MWAKA 2021/22 *SUPPLEMENTARY BUDGET*

3.1. Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 137 Ibara ndogo ya (3) inasema ikiwa katika mwaka wa fedha wowote inaonekana kwamba: Fedha za matumizi zilizoidhinishwa na sheria ya matumizi ya Fedha za Serikali kwa ajili ya shughuli fulani hazitoshi au kwamba imekuwa lazima kulipa gharama za shughuli ambayo haikupangiwa fedha za matumizi kwa mujibu wa sheria; au Kuna fedha ambazo zimetumiwa kwa ajili ya shughuli fulani kwa kiasi kinachozidi kiwango cha matumizi yaliyoidhinishwa na sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kuhusu shughuli hiyo au kwamba fedha zimetumiwa

kulipia gharama za shughuli ambayo haikupangiwa fedha za matumizi kwa mujibu wa Sheria.⁶

Mheshimiwa Spika Ibara hiyo inasisitiza Serikali kuwasilishwa kwenye Bunge makadirio ya matumizi ya nyongeza au, kadri itakavyokuwa, maelezo ya matumizi ya ziada, na baada ya Bunge kuyakubali hayo Makadirio ya matumizi ya nyongeza au maelezo ya matumizi ya ziada, kutawasilishwa kwenye Bunge Muswada wa Sheria ya Matumizi ya fedha za Serikali kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na fedha hizo zitatumia kulipia gharama za shughuli zinazohusika na hayo makadirio au maelezo.

3.2. Sheria ya Bajeti Sura ya 439

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 43 cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 Kinafafanua zaidi ibara ya 137(3) ya Katiba kwa kuweka mazingatio na utaratibu wa uwasilishaji wa *supplementary budget* Bungeni. Aidha kifungu kidogo cha 3 kinaelekeza kwamba mara baada ya Serikali kuwasilisha *supplementary budget* Bungeni itaambatana na Muswada wa Sheria ya Matumizi ili iidhinishwe na Bunge. Vilevile, Bajeti hii inayowasilishwa Bungeni ni utekelezaji wa makubaliano ambayo Serikali yetu iliingia na Shirika la Kimataifa la Fedha kwamba watawasilisha Bungeni *supplementary budget* kutokana na kupatikana kwa mkopo wa **Dola za Marekeni milioni 567.3** sawa na **Shilingi Trilioni 1.320**. Hata hivyo, kiwango kitakachowasilishwa kwenye *supplementary budget* ni **Shilingi trilioni 1,079.6⁷** na kiasi cha **shilingi bilioni 231** kimepelekwa Zanzibar.

3.3. Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/22

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu mwaka Julai-Disemba 2021/22 pamoja na

⁶ The constitution of United Republic of Tanzania of 1977

⁷ The Budget Act Cap 439

Taarifa ya Serikali ya Nyongeza ya Bajeti na kubaini kuwa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka mzima wa 2021/22 utakuwa na nakisi ya **Shilingi bilioni 704.9**. Hivyo kulikuwa na umuhimu wa kufanya marejeo ya makusanyo pamoja na utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/22 kwa sababu ya fedha za Mkopo wa IMF kutumika kutekeleza shughuli ambazo hazikuwepo kwenye Bajeti iliyokuwa imeidhinishwa pamoja na upatikanaji wa Fedha za Wafadhiri.

4.0. MGAWANYO WA FEDHA ZA MKOPO

4.1. Majadiliano baina ya Kamati ya Bajeti na Serikali

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba uliridhia Kamati ya Bunge ya Bajeti ikutane na Serikali tarehe 6 na 7 Oktoba 2021 kwa ajili ya kujadili Mpango na Mgawanyo wa Fedha za Mkopo kutoka IMF zenyenye jumla ya **Shilingi Trillioni 1.31**. Kikao hicho kilifanyika kama ulivyoelekeza na kilihusisha Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Serikali ilitoa mapendekezo ya Mgawanyo wa Fedha hizo na Kamati ilishauri masuala yafuatayo ambayo Serikali iliyakubali.

- i. Kamati ilishauri na Serikali ilikubali kufanya *reallocation* katika fedha hizo ili zipatikane fedha kwa ajili ya kujenga madarasa walau 2 hadi 5 kwa kila shule shikizi na shule za msingi zenyenye msongamano wa wanafunzi kutokana na kutokuwepo kwa madarasa. Madarasa yaliyojengwa hadi hivi sasa ni 1,155 katika maeneo yote nchi nzima.
- ii. Kamati ilishauri na Serikali ilikubali kupunguza kiasi cha **Shilingi Bilioni 40** kutoka kwenye miradi ya maji ya mijini ili zikaongezwe kwenye miradi ya maji vijijini na kufikia **Shilingi Bilioni 61** kwa kuzingatia uhitaji wa maji vijijini;
- iii. Kwa kuzingatia kuwa, fedha hizo zinatakiwa ziwe zimetumika na kumalizika ndani ya miezi 8 kuanzia mwezi Novemba. Jambo ambalo

lilionekana kuwa gumu kutekelezeka kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Manunuzi na Kanuni zake. Kamati ilishauri Serikali kutumia muongozo wa *single source* na Serikali ilikubali na ikatoa muongozo wa manunuzi kwa fedha zinazotokana na mkopo huo;

- iv. Kamati ilishauri kwamba kwa kuwa miradi inayotekelzwa haikuwa kwenye Bajeti ya Mwaka 2021/22. Hivyo, ni wazi kwamba Serikali itatakiwa kuwasilisha Bungeni *Supplementary Budget* ndio maana Serikali imetekelzeza takwa hilo la kikatiba na kisheria;
- v. Serikali ilishauriwa na ilikubali kuangalia uwezekano wa kutumia mifumo mingine ya manunuzi ya vifaa tiba kwa sababu fedha zinazoenda kutumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba ni Shilingi **Bilioni 299.34** ambayo ni zaidi ya **asilimia 100** ya Bajeti ya MSD kwa mwaka. Hivyo, uwezo wa kutumia MSD kwa muda uliopangwa wa matumizi ya fedha hizi unatakiwa kuimarishwa na kusimamiwa kwa karibu;
- vi. Serikali ilikubali kutumia mfumo wa Manunuzi wa BRN ili kupunguza mlolongo wa manunuzi. Ushauri huu ulikubaliwa na Ndio maana PPRA ilitoa muongozo wa manunuzi wa Fedha za Mkopo huo kutoka IMF;
- vii. Serikali ilishauriwa na ilikubali kupunguza ununuzi wa Advance Ambulances kutoka 48 hadi 20 na fedha zilizopatikana kiasi cha Shilingi Bilioni 7 zimetumika katika kununua Ambulances za kawaida; na
- viii. Kamati ilishauri na Serikali ilikubali kuhakikisha kwamba *Ambulances* 195 zitakazonunuliwa kuititia fedha hizi mgawanyo wake uzingatie uhitaji na umuhimu wa *Ambulance* katika maeneo husika ili zigawanywe nchi nzima.

4.2. Mgawanyo wa Mkopo baada ya Majadiliano

Mheshimiwa Spika, Baada ya majadiliano na Kamati Mgawanyo wa mwisho ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na 1 hapo chini.

Jedwali Na 1: Mgawanyo wa Fedha za Mkopo kutoka IMF

ENEKO	USD MILIONI	SHILINGI BILIONI	ASILIMIA
Maji	66.8	154.4	12.9
Afya	214.1	494.1	24.4
Elimu	125.7	290.4	28.2
MoEST	20.6	47.7	6.0
PO-RALG	105.1	242.7	18.9
Uwezeshaji wa Vijana, Wanawake na makundi yasiyojiweza	4.3	10.0	0.5
Mradi wa hifadhi ya jamii	10.8	25.5	0.5
Maliasili	43.4	100.2	8.4
Utarwala	2.2	5.0	0.3
JUMLA	567.3	1,079.6	100.0

Chanzo: Wizara ya fedha na Mipango

Mheshimiwa Spika, Katika Mgawanyo wa Fedha za Mkopo huu jumla ya Dola za Marekani **Millioni 100** sawa na **Shilingi Bilioni 231.0** zilipelekwa Zanzibar. Hata hivyo utekelezaji wake utasimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na (SMZ) Baraza la Wawakilishi.

5.0. UCHAMBUZI WA MAPENDEKEZO YA NYONGEZA YA BAJETI YA MWAKA 2021/22.

5.1. Uchambuzi wa Makusanyo

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Serikali kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kupunguzwa kwa viwango vya tozo kwenye miamala kwa **asilimia 30**, kutoanza kutekelezwa kwa utozaji tozo kwenye mawasiliano ya simu kutokana na changamoto za utekelezaji wake na kusimamishwa kwa baadhi ya ushuru wa mafuta ili kuzuia ongezeko la bei. Hivyo, matarajio ya makusanyo ya ndani yameshuka kutoka **Shilingi trilioni 22.471** hadi **Shilingi trilioni 21,778** sawa na

kushuka kwa **shilingi bilioni 693**. Mapato mengine ambayo Serikali haitaweza kufikia lengo ni Misaada na Mikopo nafuu ya Kisekta ambayo inatarajiwa kushuka kutoka **Shilingi bilioni 282.31** hadi **Shilingi bilioni 270.36** sawa na kutofikia lengo kwa **Shilingi bilioni 11,947**.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Misaada na Mikopo nafuu kutoka Washirika wa Maendeleo inatarajiwa kuongezeka kutoka **shilingi trilioni 2.956** hadi **shilingi 4.255** sawa na ongezeko la **Shilingi trilioni 1.299** ongezeko hili limetokana na upatikanaji wa Mikopo ya Biashara jumla ya **Shilingi billioni 693**. Aidha Misaada kwenye Mfuko wa Bajeti (General Budget Support) Serikali inatarajia kupokea jumla ya **Shilingi trilioni 1.310** awali Serikali haikuwa imetegemea kiasi chochote kutoka katika chanzo hiki.

5.2. Uchambuzi wa Matumizi

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kwa upande wa matumizi ya kawaida zimeongezeka jumla ya **Shilingi Bilioni 672.76** kutoka **Shilingi trilioni 23.003** zilizokuwa kwenye bajeti hadi **Shilingi Trilioni 23.676** sawa na ongezeko la **asilimia 2.9**. Fedha zilizoongezeka zimepelekwa kwenye matumizi mengineyo **Shilingi bilioni 441.764** na zilizopelekwa Zanzibar **Shilingi bilioni 231**. Kwa upande wa matumizi ya maendeleo zimeongezeka kutoka jumla ya **Shilingi trilioni 13.679** zilizokuwa kwenye Bajeti ya awali hadi **Shilingi trilioni 14.305** sawa na ongezezo la **asilimia 4.5** la **Shilingi bilioni 625.905**

Jedwali Na 2: Mapendekezo ya Nyongeza ya Bajeti kwa mwaka 2021/22

Billioni

MAPATO	BAJETI ILYOIDHINISHWA 2021/22	MAPENDEKEZO YA NYONGEZA	MABADILIKO
A. Mapato ya Ndani-Serikali Kuu	25,520,877	24,827,877	-693,000
B. Mapato ya Halmashauri	863,858	863,858	0
C. Misaada na Mikopo nafuu kutoka Washirika wa Maendeleo	2,955,923	4,254,626	1,298,703
D. Mikopo ya Ndani na Nje	7,341,240	8,034,240	693,000
JUMLA (A-D)	36,681,898	37,980,601	1,298,703
MATUMIZI			
E. Matumizi ya Kawaida	23,002,951	23,675,716	672,764
F. Matumizi ya Maendeleo	13,678,946	14,304,851	625,905
JUMLA(E+F)	36,681,898	37,980,567	1,298,669

Chanzo: Taarifa ya Wizara ya Fedha na Mipango

Mheshimiwa Spika, utaona kwamba kwenye matumizi ya kawaida zimeongezeka jumla ya Shilingi bilioni 672,764 kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 231,000 zilienda Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Shilingi bilioni 441,764 zilitumika Tanzania bara. Kamati imefanya uchambuzi wa matumizi ya shilingi billioni 441,764 na kuonekana kwamba fedha hizo zilitumika kwenye matumizi ya kawaida yenye asili ya kimaendeleo hususan katika sekta ya afya ambapo Serikali imetoe ajira kwa ajili ya kuwezesha shughuli hizo kutekelezeka na ununuzi wa madawa na chanjo.

5.3. Ujenzi wa Kipande cha Reli cha Makutopora Tabora

Mheshimiwa Spika, moja ya jambo ambalo Kamati ya Bajeti imekuwa ikishauri kila mwaka ni kuhakikisha kwamba Reli ya Kati kwa kiwango cha kisasa inakamilika pamoja na matawi yake ili faida yake ionekane. Marekebisho ya Bajeti yaliyoletwa na Serikali leo imetengwa jumla ya **Bilioni 693** kwa ajili ya kipande cha reli cha Makutopora- Tabora. Hivyo vipande vitakavokuwa vimebaki ni vya Tabora-Kaliua- Mpanda-Kalema, Tabora-Uvinza –Kogoma –Msongati. Hii ni hatua nzuri sana kwa Serikali na ni ya kupongeza.

6.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA UJUMLA

Mheshimiwa Spika, Kamati ina ushauri wa ujumla kuhusu Mkopo huo kama ifuatavyo: -

6.1. Mradi wa Ujenzi wa Vibanda vya Wafanyabiashara wadogo

Mheshimiwa Spika, Katika mgawanyo wa fedha za Mkopo huu zilitengwa shilingi Bilioni 5 kwa ajili ya ujenzi wa vibanda vya wafanyabiashara wadogo. Katika uchambuzi kamati ilibaini kwamba suala hili lilikuwa halina mpango wa utekelezaji. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha katika maeneo yote nchi nzima kuandaa mipango na kutekeleza miradi ya ujenzi wa vibanda vya wafanyabiashara wadogo ili kuondoa adha ya bomoa bomoa na kukimbizana na mgambo.

6.2. Changamoto ya Utolewaji wa Misamaha ya Kodi

Mheshimiwa Spika, pamoja na kufanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya ongezeko la Thamani Sura ya 148 kuitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021 ili kurahisisha upatikanaji wa Misamaha ya Kodi. Aidha, Serikali ilitoa kanuni kuitia gazeti la Serikali na 715 lililotolewa tarehe 8 Oktoba, 2021. Hata hivyo, hatua zote hizo bado changamoto ya utolewaji wa misamaha ya kodi inaendelea. Mfano, Kamati ilikutana na **RUWASA**

na kubaini hadi sasa kuna mabomba yamekwama bandarini kwa sababu ya kukosa msamaha wa kodi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kwenda kujipanga upya na kubaini nini hasa sababu ya kucheleweshwa kwa misamaha ya Kodi kwa sababu hadi sasa hatua zilizochukuliwa hazijaleta matunda yaliyokusudiwa.

6.3. Uwazi na Uwajibikaji kwa Mikopo inayochukuliwa na Serikali

Mheshimiwa Spika, Hatua iliyochukuliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa kulishirikisha Bunge katika mgao wa mkopo kutoka IMF Bungeni na Bunge kutoa mapendekezo yake ni hatua muhimu katika kuleta uwazi na uwajibikaji. Sote tutakubaliana kwamba mkopo huu umefuatiliwa na Waheshimiwa wabunge, Viongozi katika ngazi zote na wananchi kwa ujumla. Kamati inashauri kwenye siku za usoni kuna haja ya Serikali kuweka utaratibu huu kisheria.

7.0. PONGEJI

Mheshimiwa Spika, waswahili husema pongezi humtia mtu bidii, kwa kifupi nieleze kwanini lazima kumpongeza Mhe Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Waziri Fedha na Mipango na Ndg. Emmanuel Tutuba Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mkopo kama huu umetolewa kwa Nchi 40 za Afrika, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba nchi nyingine zimetumia mkopo huu kununua kufanya mambo ya muda mfupi kama vile kununua barakoa, kununua vipimo vya uviko, kulipia għarama za Kuweka watu karantini, kununua chanjo za uviko pamoja na mashine za Oxygen. Ni Tanzania pekee iliyotumia fedha hizi kuwekeza katika vitu vya muda mrefu ili kupambana na Uviko 19 kama vile

kuimarisha huduma za maji, barabara za utalii, Miundombinu ya Msingi ya Afya. Hatua hii ni muhimu kwa sababu ugonjwa wa Uviko upo na tutaishi nao hivyo ni lazima kuwekeza katika vitu vya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Mkopo wa **Dola za marekani milioni 567.39** Ulikuwa umegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza, ni asilimia moja ya tatu ya mkopo sawa na **Dola za marekani milioni 189.1** zilikuwa zitozwe riba ya **asilimia 1.05** kwa kipindi cha miaka 10 baada ya kumalizika kwa muda wa neema (*Grace period*) wa Miaka 5. Sehemu ya pili, ya mkopo ilikuwa ni theluthi mbili ya mkopo sawa na **Shilingi milioni 378.2** ilikuwa zirejeshwe kwa miaka 10 bila riba. Baada ya Shirika la Fedha la kimataifa kuona kasi na utekelezaji wa miradi inayotokana na mkopo huu waliamua kusamehe riba yote hivyo, mkopo huu utarejeshwa kwa miaka 10 bila riba mara baada ya kipindi cha neema kumalizika.

Mheshimiwa Spika, ninaweza kuendelea kutoa pongezi hizi mpaka Bunge lako Tukufu lisihairishwe siku ya leo, nimalizie tu kwa kusema kwa yanayoendelea Watanzania wasubirie mema zaidi.

8.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru na kukupongeza kwanza wewe Mheshimiwa Spika Dkt Tulia Ackson, (Mb) kwa kunipa fursa ya kuwasilisha Taarifa hii. Vilevile, nimpongeze Mussa Azzan Zungu, (Mb) Naibu Spika kwa kukusaidia vyema Mheshimiwa Spika. Pili, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, (Mb) Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Naibu Waziri Hamad Hassan Chande (Mb). kwa ushirikiano wao ambao wamekuwa wakitoa kwa Kamati katika kipindi chote cha vikao vya Kamati. Nawashukuru pia wataalam wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kutekeleza shughuli za Kamati. Aidha, nawapongeza kwa michango yao, maoni na ushauri ambayo imesaidia katika kuhakikisha kuwa Kamati inasimamia Serikali ipasavyo. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb
4. Mhe. Issa Jummanne Mtemvu, Mb
5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
6. Mhe. Josephati Sinkamba Kandege, Mb
7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb
8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb
9. Mhe. Shally Josepha Raymomd, Mb
10. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
11. Mhe. Subira Khamis Mgatu, Mb
12. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb
13. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb
14. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb
15. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb
16. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
17. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb
18. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb
19. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb
20. Mhe. Halima James Mdee, Mb
21. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb
22. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb
23. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretarieti yote ya Bunge chini ya Uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati, Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Mathew Kileo, Makatibu wa Kamati Ndg. Emmanuel Rhobi, Ndg. Maombi Kakazi na Ndg. Wilfred Akasi kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Idara na Vitengo katika Ofisi ya Bunge, kwa kuhakikisha kwamba shughuli za Kamati zinafanyika kama zilivyokuwa zimepangwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa lipokee na kujadili na hatimaye kuitisha mapendelekezo ya Serikali kuhusu Mapendelekezo ya Nyongeza ya Bajeti ya Mwaka 2021/22.

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Daniel Baran Sillo, Mb

MWENYEKITI

KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

18 Februari, 2022